

PROCUREMENT AND SUPPLIES PROFESSIONALS AND TECHNICIANS BOARD

Telephone: 022 2865860
Tel/fax: 022 2862138
Website: <http://www.psptb.go.tz>



P.O. Box 5993
Dar es Salaam.
E-mail: info@psptb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Bodi ya Wataalam wa ununuzi na ugavi (PSPTB) imetunukiwa tuzo ya viwango vya kitaaluma na International Federation of Purchasing and Supply Management (IFPSM) na kutambulika kimataifa kwa kukidhi viwango vya kimataifa.

Tuzo hiyo ilitolewa kwa PSPTB katikati ya mwezi Februari 2016 imeifanya PSPTB kuwa bodi ya kwanza Barani Afrika kupata tuzo hiyo ya viwango vya kimataifa kutoka IFPSM. Haya ni matokeo chanya ya ufanyaji kazi kwa bidii na juhudi zilizoonyeshwa na Bw. Tesha, Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB akishirikiana na timu yake ya PSPTB.

Kwa niaba ya mwenyekiti wa bodi ya wataalam wa viwango vya kimataifa Dkt. Paul Davi, Rais wa IFPSM Bw. Cheryl Paradowski na Mkurugenzi Mtendaji wa IFPSM Bw. Malcolm Youngson rasmi wameipongeza PSPTB kwa kazi kubwa walioifanya na kuwa taasisi ya kwanza barani Afrika kufikia kiwango hicho na kutambuliwa kimataifa kwenye taaluma hii.

Kabla ya kupata Tuzo hiyo, PSPTB ilisajiliwa kama mwanachama mhusishwa na IFPSM mwaka 2015. Bw. Tesha amesisitiza kuwa PSPTB itaendelea kufanya vizuri ili itunze heshma hiyo iliyopata na kuendelea kuwa mfano wa kuigwa katika bara la Afrika kama maono ya PSPTB yanavyojieleza.

Aidha Bw. Tesha amesema, PSPTB ilizindua mtaala mpya wa mafunzo mnamo Disemba, 2015. Mtaala huo kwa sasa unaendelea kufundishwa katika vituo mbalimbali vya maandalizi ya mitihani ya Bodi, ambapo mitihani ya kwanza chini ya mtaala huu mpya, utafanyika November 2016.

Ameeleza mambo muhimu katika mtaala huo ni pamoja na utaratibu wa kuanzisha masomo ya usimamizi wa ununuzi wa umma kuanzia ngazi za chini hadi juu. Pia, mtaala huu umesisitiza utaratibu wa kutakiwa kufaulu ngazi yoyote ya mtihani ndani ya miezi ishirini na nne (24) toka mtahaniwa afanye mtihani kwa mara ya kwanza kwa kila ngazi/ hatua.

Hata hivyo mtaala huu umetoa nafuu kwa watahiniwa ambapo kuanzia sasa, kila somo mtahiniwa atakalo faulu litarekodiwa hatakama amefaulu moja na kufeli mengine, atatakiwa kufaulu hayo mengine ndani ya miezi ishirini na nne (24).

Shamim Ally Mdee

Afisa Mwandamizi wa Masoko na Mahusiano ya Umma- PSPTB

Dar es Salaam

05 Mei, 2016.